


Bibilia ya watoto
Inawalettea

Yesu
Anyamazisha
Dhoruba
Baharini



Kimeandikwa na: Edward Hughes

Kimeorodheshwa na: Janie Forest
Alastair Paterson

Imerekebishwa na: Ruth Klassen

Kimetafsiriwa na: Bethel Children's Home,
Kisumu, Kenya and Emmanuel Menya

Kimedhibitishwa na: Bible for Children
www.M1914.org

©2020 Bible for Children, Inc.

License: Kuna ruhusa ya kuchapa hadithi hii, lakini bila ya kuuza.





Yesu na wanafunzi
Wake walikuwa
kwenye mashua
ilipotokea dhoruba
kubwa. Iileta
msukosuko mkuu
katika Bahari ya
Galilaya. Aina hii
ya dhoruba
ingeweza
kusababisha
kuharibika na
kuzama kwa
mashua.



Dhoruba iliwaogofya wanafunzi. Mawimbi yaliifunika mashua, na kuijaza maji.



Lakini Yesu alikuwa amelala akiwa salama kabisa katikati ya dhoruba. Wanafunzi wakamuamsha Yesu wakilia, "Bwana, Bwana, tunaangamia!"




Yesu akawauliza wanafunzi Wake, "Kwanini mmekuwa waoga, enyi wa imani haba?" Kisha Yesu akaamuru upepo unyamaze ... Na ... Yesu akaamuru mawimbi yatulie na kunyamaza ...



NA UPEPO UKANYAMAZA ... BAHARI IKAWA
SHWARI NA KIMYA.

Wanafunzi wakamaka, wakisema, "Huyu ni mtu wa
aina gani hata pepo na bahari zamtii!"




Muda fulani baadaye,
Yesu akawa na siku yenye
shughuli nyingi. Zaidi ya
watu 5000 walimfuata
hadi sehemu ya jangwa.




Kwa uwezo wa Mungu, Yesu akalisha umati wote kwa kutumia chakula kidogo kinachotosha kulisha mlo mmoja kwa kijana mdogo. Sasa ilikuwa jioni. Yesu akaagana na watu waende zao.



Hata wanafunzi walitakiwa kuondoka. Yesu akawaacha wapande mashua na kumtangulia upande wa pili wa Bahari ya Galilaya.





Alipowaaga watu
wote waende zao,
Yesu akapanda
mlimani peke yake
ili kuomba.
Ilipofika jioni,
akawa peke yake
huko.





Huko ziwani, wanafunzi
wakakabiliana na
upepo mkali.

Upepo ukawazuia
kuvuka, ingawa
walipiga
makasia
kwa
masaa.

Wanafunzi
hawakujua,
lakini wakapata
mshangao
mkubwa!





Muda fulani kati ya saa tisa na saa kumi na mbili asubuhi, katikati ya bahari iliyochafuka, wanafunzi waliona kitu kilichowatia hofu. Wakalia, "Ni kivuli!" Lakini alikuwa ni Yesu, Bwana wao, alikuwa anakuja kwao, **AKITEMBEA JUU YA MAJI.**



Yesu akawaambia,
"Jipeni moyo. Ni
mimi; msilogope."
"Bwana, kama ni
Wewe, niamuru nije
kwako juu ya maji."
Hivyo Yesu akasema,
"Njoo." Kwa uhodari,
Petro akashuka
chomboni akatembea
juu ya maji
kumuelekea Yesu.





Lakini Petro
alipoona upepo
unavuma,
akaogopa, na
kuanza kuzama.
Akalia. "Bwana,
niokoe!"



Mara, Yesu akanyosha mikono yake na kumshika Petro. Akamuuliza, "Ewe mwenye imani haba, mbona uliona shaka?" Na Petro na Bwana Yesu walipopanda chomboni, upepo ukakoma.



Kisha wale waliokuwa
kwenye mashua wakaja
na kumsujudia Yesu,
wakisema, "Hakika
Wewe ni Mwana wa
Mungu."



Yesu Anyamazisha Dhoruba Baharini

Hadithi kutoka kwa Neno la Mungu, Bibilia,

inapatikana katika

Mathayo 8, Mathayo 14,
Marko 4, Luka 8

"Kufafanusha maneno yako kwatia nuru."

Zaburi 119:130



Mwisho



Hii hadithi ya bibilia inatueleza kumhusu Mungu wetu wa ajabu aliyetuumba na anayetaka tumjue.

Mungu anajua tumetenda mambo mabaya, anayoyaita dhambi. Adhabu ya dhambi ni mauti, lakini Mungu anakupenda sana hata akamtuma mwana wake wa pekee, Yesu, Ili afe msalabani na aadhibiwe kwa dhambi yako. Alafu Yesu akafufuka na kuenda nyumbani mbinguni! Ukimwamini Yesu na kumwomba msamaha kwa dhambi yako, Atakusamehe! Yesu atkuja na kuishi ndani yako, na utaishi naye milele.

Kama unaamini huu ni ukweli, Sema haya kwa Mungu: Mpendwa Yesu, ninaamini kuwa wewe ni Mungu, na ulifanyika mtu ili ufe kwa ajili ya dhambi zangu, ili niwe na maisha mapya, na siku moja nitaenda kuwa nawe millele. Nisaidie nikutii na niishi kwa ajili yako kama mtoto wako. Amina.

Soma bibilia na uzungumze na Mungu kila siku! Yohana 3:16

